**HOTUBA YA MGENI RASMI KATIKA SHUGHULI YA UTOAJI HUNDI ZA MIKOPO YA WANAWAKE**

- Ndugu Mkurugenzi Mtendaji;
- Wadau toka taasisi mbalimbali
- Kamati ya mikopo ya Wilaya;
- Maafisa Maendeleo ya Jamii;
- Wanavikundi Wote;
- Wageni Waalikwa ,Mabibi na Mabwana;

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kutuwezesha kuiona siku hii ya leo.

Napenda kuchukua nafsi hii kuwapongeza Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri wanazofanya katika kuhakikisha maendeleo na Ustawi wa wananchi unafikiwa.

**Katika siku ya leo nina majukumu makubwa mawili,moja ni kuwakabidhi mikopo ya wanawake na vijana lakini pia jukumu kubwa nililonalo ni kuzindua jukwaa la wanawake la wilaya.**

**MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA:**

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya kwa kuona umuhimu wa kuviwezesha vikundi vya wanawake na vijana kwa kuvipa mikopo yenye masharti nafuu.Vile vile nichukue fursa hii kuwapongeza Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata kwa kuvilea vikundi na hatimae kuwa na sifa za kupata mikopo hii.

Nafurahi kusikia kwamba mikopo hii imewafikia watu wa makundi mbalimbali kama vile walemavu, wajane, wanawake na waathirika wa ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Mikopo imesaidia kuinua hali za kiuchumi kwa makundi hayo kwani walengwa wa mikopo hii wameboresha shughuli zao za uzalishaji mali, hii ni kutokana na riba ndogo inayotozwa na mifuko hii yaani asilimia 10% kwa mwaka ukilinganisha na riba inayotozwa na vyombo vingine vya fedha.

Nafurahi kusikia Kwa sasa mifuko hii inajiendesha yenyewe, hii ni kutokana na riba inayotozwa pamoja na michango ya Halmashauri inayochangia kwa asilimia kumi ya kila mapato yake kwa mifuko yote hivyo haitegemei fedha toka Wizarani. Mpaka sasa mifuko hii ina mtaji usiopungua Tsh 257,830,136.00/= napenda kuipongeza Halmashauri ya Wilaya Mbeya kwa niaba ya Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa juhudi na mikakati yao ya kuweza kukuza mtaji wa mifuko hii.

Ni matarajio yangu kuwa mikopo hii itatumika kama ilivyotarajiwa ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa na kutekeleza Sera ya Maendeleo na Ilani ya Chama Tawala inayotutaka kuwezesha wananchi kiuchumi ili kujiletea maendeleo endelevu.

Pia naomba nichukue fursa hii kuwapongeza wanavikundi mliobahatika kupata mikopo siku ya leo kwani nimesikia kuwa Halmashauri ina vikundi visivyopungua 210 vilivyo hai kati ya hivi, vikundi 31 vya wanawake vinakabidhiwa mkopo leo yenye jumla ya Tsh 121,000,000/= na vikundi 15 vya vijana vinakabidhiwa mkopo wa Tsh 53,000,000/= Vikundi hivi vinatoka katika kata 15 kati ya kata 28. Naamini kuwa vikundi hivi vimechanguliwa kwa kuzingatia vigezo muhimu vilivyowekwa na Wizara husika.

Hivyo basi ni matumaini yangu mikopo hii mlipata leo itaanza kurejeshwa mara tu baada ya kuisha kipindi cha siku 30 kwa kufuata utaratibu mliowekewa na kuzingatia vipengele vyote vilivyosainishwa kwenye mkataba wa mikopo hii.

Kumbukeni kuwa mikopo hii sio Zawadi hivyo basi ni vema ikarejeshwa kwa wakati ili kuwawezesha wengine kunufaika na mikopo hii. Vilevile sitegemei kuona kikundi chochote kinachukuliwa hatua za kisheria kutokana na kushindwa kurejeshwa kwa wakati.

## UZINDUZI WA JIKWAA LA WANAWAKE LA WILAYA:

Uanzishwaji wa majukwaa ya wanawake umekuja baada ya kutambua kuwa wanawake wamekuwa hawapati fursa za kutosha za kiuchumi hapa Tanzania na hata Duniani kote na hii inatokana na kutokuwa na usawa katika fursa, uwezo wa kupata mitaji, ajira na baadhi ya maeneo malipo ya kazi kwa wanawake yamekuwa sio sawa na wanaume. Kuondoa matabaka na sheria ambazo zitasaidia kuondoa ubaguzi wa kiuchumi kwa wanawake ni jambo la muhimu sana katika kuleta maendeleo ya usawa katika pato la taifa, jamii na familia. Ushiriki wa wanawake katika uchumi unaleta mabadiliko makubwa sana katika familia, jamii na nchi kwa ujumla.

Katika kusaidia kufikia malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo pia yamesisistiza Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliteua timu ya viongozi na wataalam akiwemo Mhe. Makamu wa Rais Mama Samia Hassan Suluhu ambao watafanya kazi kama chombo cha juu katika kutambua na kuweka mikakati ya kupunguza na kuondoa pengo kubwa ambalo limejengeka duniani na kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchumi duniani kote.

Uwezeshaji wanawake kiuchumi ni muhimu kwa kuhakikisha malengo ya maendeleo endelevu na Malengo ya 50/50 ya Dunia yanafikiwa ifikapo mwaka 2030. Kufuatia

umuhimu huu Mhe. Makamu wa Rais Mama Samia Hassan Suluhu ameelekeza kuwepo kwa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Mikoa na Halmashauri zote za Tanzania, kwani majukwaa haya yatasaidia kuongeza uelewa wa wanawake katika uchumi, biashara, upatikanaji wa mitaji, sheria za nchi katika masuala ya uchumi na jinsi ya kujitegemea kiuchumi.

Serikali imeweza pia kuanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wanchi Kiuchumi ambalo linasimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuwaongoza Watanzania kwenye uchumi imara kwa kuhakikisha kunakuwepo mazingira mazuri ya biashara na uchumi shirikishi.

Kwa kuliona suala hili la uwezeshaji kwa umuhimu wake Halmashauri ya wilaya ya mbeya imelitekeleza hili kwa kufanya mambo yafuatayo:

- Kuhamasisha wanawake kuunda vikundi vya kiuchumi ili kukusanya mawzo na kujiletea maendeleo yao wenyewe
- Kutoa mafunzo ya ujariamali,umuhimu wa vikundi,utunzaji wa kumbukumbu,matumizi sahihi ya fedha za ndani pamoja na mikopo na uimarishaji wa vikundi
- Kuwaunganisha wanawake na taasisi binafsi kama vile CARITAS ili kujipatia fursa nyinginezo.
- Kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili kufikia 50/50
- Sambamba na hilo, halmashauri imeendelea kusimamia kikamilifu Mfuko wa Wanawake (WDF) ili kuviwezesha vikundi vya wanawake kwa kuvipatia mikopo yenye riba nafuu ya asilimia kumi (10%) kwa ajili ya kuendeshea shughuli za ujasiriamali.
- Uwezeshaji wa mikopo yenye riba nafuu

Katika kutekeleza adhima ya serikali ya kufikia Malengo ya Maendeleo Undelevu na Malengo ya 50/50 ya Dunia ifikapo mwaka 2030, natamka rasmi kuwa **JUKWAA LA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI LA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA limezinduliwa.**

Niwatakie shughuli njema za uzalishaji ili kuleta maendeleo katika ngazi ya familia zenu, Kata, Halmashauri yetu na Taifa kwa ujumla.

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA***